TAARIFA YA MAELEZO YA CHANJO

# Chanjo ya Homa ya Manjano A

*Unachohitaji Kujua*

Many Vaccine information Statements are available in Spanish and other languages. See www.immunize.org/vis

Hojas de información sobre vacunas están disponibles en español y en muchos otros idiomas. Visite www.immunize.org/vis

## 1 Kwa nini nipokee chanjo?

Homa ya manjano ni ugonjwa mkali wa ini. Husababishwa na kirusi cha homa ya manjano A (HAV). HAV husambazwa kutoka mtu mmoja hadi mtu mwingine kupitia ugusaji wa kinyesi cha watu walioathiriwa, jambo linaloweza kufanyika kwa urahisi ikiwa mtu hataosha mikono yake vizuri. Pia unaweza kupata homa ya manjano A kutoka kwa chakula, maji, au vitu vyenye HAV.

Dalili za homa ya manjano A zinajumuisha:

- homa, uchovu, kukosa hamu ya chakula, kichefuchefu, kutapika, na/au maumivu ya viungo
- maumivu makali ya tumbo na kuharisha (hasa katika watoto), au
- umanjano (ngozi na macho ya manjano, mkojo mweusi, choo cha rangi ya udongo).

Kwa kawaida dalili hizi huonekana wiki 2 hadi 6 baada ya kuathiriwa na hupotea ndani ya miezi 2, ingawa watu wengine wanaweza kuwa wagonjwa kwa zaidi ya miezi 6. Ikiwa una homa ya manjano A unaweza kuwa mgonjwa kufanya kazi.

Mara nyingine watoto huwa hawaonyesho dalili, lakini watu wengi wakubwa huonyesha. Unaweza kusambaza HAV bila kuwa na dalili.

Homa ya manjano A inaweza kusababisha matatizo ya ini na kifo, ingawa jambo hili ni nadra na hutokea mara kwa mara kwa watu wenye umri wa miaka 50 au zaidi na watu wenye magonjwa mengine ya ini, kama vile homa ya manjano B au C.

**Chanjo ya homa ya manjano A inaweza kuzuia homa ya manjano A.** Chanjo za homa ya manjano zilipendekezwa Marekani kuanzia 1996. Tangu wakati huo, idadi ya kesi zilizoripitwa kila mwaka nchini Marekani zimepungua kutoka takriban kesi 31,000 hadi chini ya kesi 1,500.

## 2 Chanjo ya Homa ya Manjano A

Chanjo ya homa ya manjano A ni chanjo isiyo hai (iliyouliwa). Utahitaji **dozi 2** kwa kinga ya kudumu muda mrefu. Dozi hizi zinafaa kupeanwa kati ya angalau miezi 6.

Watoto hupewa chanjo mara kwa mara kati ya siku ya kwanza ya kuzaliwa na siku ya pili ya kuzaliwa (umri wa miezi 12 hadi miezi 23). Watoto wakubwa na vijana wanaweza kupewa chanjo baada ya miezi 23. Watu wazima ambao hawajapokea chanjo hapo awali na wanataka kulindwa kutokana na homa ya manjano pia wanaweza kupokea chanjo.

Unafaa kupata chanjo ya homa ya manjano ikiwa:

- unasafiri kuenda katika nchi ambapo visa vya homa ya manjano A hutokea mara kwa mara,
- wewe ni mwanamume anayefanya ngono na wanaume wengine,
- unatumia dawa za kulevya,
- una ugonjwa hatari wa ini kama vile homa ya manjano B au homa ya manjano C,
- unatibiwa na vikoleza vya kugandisha damu,
- unafanya kazi na wanyama waliathiriwa na homa ya manjano A au katika maabara ya utafiti wa homa ya manjano A, au
- unatarajia kushirikiana na mtu aliyeasili mtoto kutoka nchi ambapo visa vya homa ya manjano A hutokea mara kwa mara

Muulize mtoa huduma wako wa afya ikiwa unataka maelezo zaidi kuhusu makundi yoyote kati ya makundi haya.

Hakuna hatari zinazojulikana za kupokea chanjo ya homa ya manjano A kwa wakati mmoja na chanjo zingine.

## 3 Baadhi ya watu hawafai kupokea chanjo hii

Mjulishe mtu anayekupa chanjo:

- **Ikiwa una mizio yoyote mikali ya kutishia maisha.** Ikiwa ushawahi kuwa na mzio wa kutishia maisha baada ya dozi ya chanjo ya homa ya manjano A, au unapata mzio mkali wa sehemu yoyote ya chanjo hii, huenda ushauriwe usipokee chanjo hiyo. Muulize mtoa huduma wako wa afya ikiwa unataka maelezo kuhusu viungo vya chanjo.



U.S. Department of Health and Human Services
Centers for Disease Control and Prevention

- **Ikiwa huli vizuri.**
  Ikiwa una ugonjwa usio mkali, kama vile homa, kuna uwezekano ukapokea chanjo yako leo. Ikiwa wewe ni mgonjwa kiasi au sana, labda unafaa kusubiri hadi upone. Daktari wako anaweza kukushauri.

## 4 Hatari za mzio wa chanjo

Ukitumia dawa zozote, hata chanjo, huwa kuna uwezekano wa madhara. Madhara haya huwa kidogo na hupotea yenyewe, lakini mizio hatari pia inawezekana.

Watu wengi wanaopata chanjo ya homa ya manjano A huwa hawapati matatizo yoyote nayo.

**Matatizo yasiyo makali** baada ya kupokea chanjo ya homa ya manjano A yanajumuisha:
- maumivu au wekundi kwenye sehemu iliyodungwa sindano
- choma kidogo
- maumivu ya kichwa
- uchovu

Ikiwa matatizo haya yatatokea, huanza mara tu baaada ya kupokea sindano na huchukua siku 1 au 2.

Daktari wako anaweza kukuarifu zaidi kuhusu mizio hii.

**Matatizo mengine yanayoweza kutokea baada ya chanjo yoyote:**

- Wakati mwingine watu huzimia baada ya utaratibu wa matubabu, ikiwa ni pamoja na chanjo. Kuketi au kulala chini kwa takriban dakika 15 kunaweza kusaidia kuzuia kuzirai, na majeraha yanayosababishwa na kuanguka. Mwambie daktari wako ikiwa unahisi kizunguzungu, au kubadilika kwa namna unavyoona au kelele katika masikio.
- Baadhi ya watu hupata maumivu ya bega yanayoweza kuwa makali na kudumu muda mrefu kuliko maumivu ya kawaida yanayosababishwa na sindani. Jambo hili hufanyika mara chache sana.
- Dawa zozote zinaweza kusababisha mzio mkali. Mizio kama hii kutoka kwa chanjo huwa nadra sana, inakadiriowa takriban dozi 1 kati ya dozi milioni moja, na inaweza kutokea ndani ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

Kama tu dawa zozote, kuna nafasi ndogo sana ya chanjo kusababisha majeraha makali au kifo.

Usalama wa chanjo hufuatiliwa wakati wote. Kwa maelezo zaidi, tembelea: **www.cdc.gov/vaccinesafety/**

## 5 Na kukiwa na tatizo hatari?

**Ninafaa kutafuta nini?**
- Tafuta kitu chochote kinachokutua wasiwasi, kama vile dalili za mzio mkali, homa kali sana, au tabia isiyo ya kawaida.

Dalili za **mzio mkali** zinaweza kujumuisha mabaka ngozini, uvimbe usoni na kwenye koo, ugumu wa kupumua, mapigo ya kasi ya moyo, kizunguzungu, na udhaifu. Dalili hizi huanza baada ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

**Ninafaa kufanya nini?**
- Ikiwa unafikiria ni **mzio mkali** au jambo lingine la dharura ambalo haliwezi kusubiri, piga simu kwa 9-1-1 au nenda katika hospitali iliyo karibu nawe. La sivyo, piga simu kwenye kliniki yako.

Baadaye, mzio unafaa kuripotiwwa Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo (VAERS). Daktari wako anafaa kutoa ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe kupitia tovuti ya VAERS katika **www.vaers.hhs.gov**, au kwa kupiga simu kwa **1-800-822-7967**.

*VAERS huwa haitoi ushauri wa kimatibabu.*

## 6 Programu ya Fidia ya Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa

Programu ya Fidia ya Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa (VICP) ni programu ya shirikisho iliyoundwa kuwafidia watu ambao huenda wakawa wamejeruhiwa na chanjo fulani.

Watu wanaoamini wamejeruhiswa na chanjo wanaweza kupata maelezo kuhusu programu hii na kuhusu kuripoti madai kwa kupiga simu kwa **1-800-338-2382** au kutembelea tovuti ya VICP katika **www.hrsa.gov/vaccinecompensation**. Kuna kikomo cha muda wa kuripoti madai ya fidia.

## 7 Ninaweza kupata maelezo zaidi aje?

- Muulize mtoa huduma wako wa afya. Anaweza kukupatia kipeperushi cha furushi la chanjo au kupendekeza vyanzo vingine vya maelezo.
- Piga simu kwa idara ya afya iliyo karibu na wewe au ya jimbo.
- Wasiliana na Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (CDC):
  - Piga simu kwa **1-800-232-4636** (**1-800-CDC-INFO**) au
  - Tembelea tovuti ya CDC katika **www.cdc.gov/vaccines**

Vaccine Information Statement
Hepatitis A Vaccine - Kiswahili
7/20/2016
42 U.S.C. § 300aa-26
Office Use Only
Translation provided by Minnesota Department of Health